# Viwango vya Bodi katika Jimbo la Washington

## Utangulizi

Hati hii inatoa muhtasari wa viwango muhimu vya **hisani, zisizo za faida, zisizo-za bodi wanachama** chini ya **sheria za jimbo**, Sheria ya Washington Nonprofit Corporation Act, kuanzia Januari 1, 2022. Inakusudiwa kutoa mwongozo wa jumla kuhusu mahitaji kwaajili ya bodi za kujichagulia. Pia inaangazia mashirika ya kutoa misaada yasiyo ya faida: mashirika yasiyo ya faida ambayo yanaendeshwa kimsingi au kipekee kwa dhumuni moja au zaidi ya kutoa misaada ambayo yanaweza kulipa sifa shirika hadhi ya msamaha wa kodi chini ya Kifungu cha 501(c)(3) cha Kanuni ya Mapato ya Ndani.  Hati hii haitambulishi uanachama mashirika yasiyo ya faida au sheria ya shirikisho (angalia Mwongozo wa Mashirika Yasiyo ya Faida Washington  kwa maelezo zaidi).

### Soma zaidi:

Sheria ya Shirika lisilo la faida Washington: RCW (24.03A)

Ufafanuzi: RCW 24.03A.010(5)&(6)

Maelezo haya yametolewa ili viongozi wote wasio wa faida waweze kuelewa mahitaji muhimu ya kisheria ya jimbo kwa bodi zisizo za faida. Baadhi ya wasomaji wanaweza kushangazwa kwa baadhi ya mikataba ambayo walidhani kuwa ni mahitaji ya kisheria kumbe ni ya hiari. Kwa bodi zinazopenda kubuni au kusambaza uongozi kwa mapana zaidi ndani ya shirika lao, inaweza kuwa uhuru kujifunza kwamba baadhi ya majukumu yanaweza kukabidhiwa kwa wafanyakazi au kamati za ushauri, au kwamba sheria hailazimishi matumizi ya mbinu maalum ya kufanya maamuzi. Taarifa hii inaweza kutumika kutambua ni kazi gani bodi inapaswa kufanya, na ni nini kinachoweza kukabidhiwa, kushirikiwa, au kufanywa na wengine. Kwa maelezo zaidi kuhusu uongozi mbadala, angalia Zana za Uongozi Mbadala.

## Kanusho

Hati hii ni kwa madhumuni ya kielimu pekee. Haikusudiwi kuwa pana, na kwa vyovyote maudhui haya hayatachukuliwa kuwa ya kisheria, biashara, au ushauri wa kitaalamu au shauri. Pia hayatengenezi uhusiano wa wakili na mteja. Kwa ushauri wa kisheria tafadhali wasiliana na wakili aliyeidhinishwa.

Kwa ujumla, sheria ya jimbo inafafanua vigezo vya viwango vya bodi, na sheria ndogo zinaweza kutungwa ndani ya vigezo. Ikiwa sheria ndogo za shirika lisilo la faida ziko kimya juu ya suala fulani, Sheria ya Shirika la Mashirika Yasiyo ya Faida la Washington litatoa kiwango cha msingi. Hati hii inatumia misamiati "wajumbe wa bodi" na "wakurugenzi" kwa kubadilishana.

*Hati hii ilitayarishwa kwa ushirikiano na Communities Rise na kuwezeshwa kwa usaidizi wa Ofisi ya Jimbo la Washington ya Katibu wa Jimbo.*

Nonprofit Association of Washington

WASHINGTON Secretary of State Corporations & Charities Division

COMMUNITIES RISE

APEX LAW GROUP


©2022 Muungano wa Mashirika Yasiyo ya Faida Washington
Haki zote zimehifadhiwa.



**Board Members/ Directors**

| Wajumbe wa bodi/Wakurugenzi | Kanuni Iliyorekebishwa ya Sehemu ya Washington (kiungo) |
|---|---|
| • Wanachama wa bodi/wakurugenzi lazima wawe watu binafsi na hawahitaji kuwa wakaazi wa Jimbo la Washington. Sheria ndogo zinaweza kuongeza sifa za ziada kama ilivyokubaliwa na wajumbe wa sasa wa bodi. | 24.03A.500 |
| • 501(c)(3) mashirika umma ya kutoa misaada ya lazima yawe na angalau wajumbe 3 wa bodi. | 24.03A.505(2) |
| • Vijana wa umri chini ya miaka 18 wanaweza kutumika katika bodi. Bodi inweza kuwa na wakurugenzi vijana 3, au ⅓ ya jumla ya idadi wakurugenzi katika bodi inaweza kuwa vijana – idadi yoyote iliyo ndogo. | 24.03A.505(3) |
| • Urefu wa muda wa bodi kwa chaguomsingi ni mwaka 1, isipokuwa kama sheria ndogo zitaeleza tofauti. Muda wa juu zaidi wa bodi kwa wajumbe wa bodi waliochaguliwa na wajumbe wengine wa bodi ni miaka 5. | 24.03A.515(1)<br>24.03A.515(1) |
| • Sheria haina kiwango cha juu cha idadi ya muda ambao mkurugenzi anaweza kutumikia. Sheria ndogo zinaweza kubainisha vikomo vya muda. | |
| • Mwanachama wa bodi anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa maneno ya mdomo katika mkutano wa bodi au kwa maandishi kwa rais, katibu au afisa mwingine aliyeteuliwa, kama ilivyoelezwa katika sheria ndogo za shirika. | 24.03A.525(1) |
| • Ikiwa muda wa mkurugenzi umeisha, mkurugenzi ambaye muda wake ndio umeisha anaendelea kutumikia hadi pale mrithi wake atakapochaguliwa, isipokuwa sheria ndogo zinaeleza tofauti. | 24.03A.515(6) |
| • Utaratibu wa kumwondoa mjumbe wa bodi hauhitaji kuingizwa kwenye sheria ndogo. Angalia sheria kwaajili ya taarifa maalum | 24.03A.530 |



**Officers**

| Maafisa | |
|---|---|
| • Maafisa wanaohitajika ni rais, katibu na mweka hazina. Ofisi ya makamu wa rais haihitajiki | 24.03A.585(1) |
| • Ofisi mbili zinaweza kushikiliwa na mtu mmoja, isipokuwa ofisi za rais na katibu lazima ziwe na watu tofauti. | 24.03A.585(3) |



**Committees**

## Kamati

- Kamati za bodi zinaweza kuwa zimekabidhi mamlaka kutoka kwa bodi kufanya maamuzi, kwa mfano, Kamati ya Utendaji. Lazima kuwe na angalau wanachama 2 wa bodi, na ni wajumbe wa bodi pekee ndio wanaweza kutumika kama wajumbe wa kamati ya kupiga kura. — 24.03A.575(1)&(4)
- Kuna mambo mengi kamati ya bodi haiwezi kuyafanya: kuidhinisha ugawaji, kubadilisha sheria ndogo au vifungu, kufanya maamuzi juu ya nani ni mjumbe wa bodi au mjumbe wa kamati ya bodi, kuidhinisha mabadiliko makubwa ya muundo wa shirika (kama vile kuunganishwa, kuuza kiasi kikubwa cha mali, kufutwa, nk), au kubadilisha azimio la bodi isipokuwa kwa kuruhusiwa na azimio la bodi. — 24.03A.575(5)
- kamati za ushauri hazina mamlaka kamili kutoka kwenye bodi na haziwezi kufanya maamuzi kwa niaba ya bodi Wanatoa mapendekezo na kutoa taarifa kwa bodi au kufanya kazi isiyohitajika kufanywa na bodi, kama vile kuandaa tukio, kuajiri watu wa kujitolea, au kuandaa tathmini ya mpango. Mtu yeyote kutoka katika jumuia anaweza kutumika katika hiyo kamati, vinginevyo iwe imeelezwa katika sheria ndogondogo — 24.03A.575(7)



**Decision-Making**

## Ufanyaji maamuzi

- Ikiwa haijajumuishwa katika sheria ndogo, akidi ni wajumbe wengi wa bodi walio ofisini kabla ya mkutano/kikao kuanza. Sheria ndogo zinaweza kutoa mahitaji ya juu ya akidi (kama vile makubaliano), lakini sheria ndogo haziwezi kuruhusu akidi kuwa chini ya ⅓ ya idadi ya wakurugenzi kwenye bodi. Akidi inahitajika kufanya maamuzi. — 24.03A.565(1) 24.03A.565(2)
- Sheria hairuhusu wajumbe wa bodi kujitokeza kwa kutumia wakala (kuruhusu mtu mwingine kufanya kwa niaba yao). — 24.03A.565(5)
- Kura iliyoandikwa kwa barua pepe au rekodi nyingine iliyoandikwa inaweza tu kutokea ikiwa kuna ushiriki wa 100% wa wanachama wote wa bodi ambao hawajagombana, na kila mjumbe wa bodi anakubali kwa uthabiti hatua iliyopendekezwa. — 24.03A.570
- Bodi inaweza kuendesha mikutano kwa kutumia njia moja au zaidi ya mawasiliano ya mbali (kama vile Zoom au programu ya mikutano ya kimtandao) ambapo wakurugenzi wote wanaweza kushiriki kwa wakati mmoja wakati wa mkutano. — 24.03A.550

**Fiduciary**

## Wajibu wa Uaminifu au Viwango vya Maadili

| | |
|---|---|
| ● Wanapotumikia kwenye bodi isiyo ya faida, wakurugenzi na maafisa wa bodi wana wajibu wa utunzaji/kujali, utii na uaminifu kwa shirika lisilo la faida. Wakurugenzi na maafisa lazima wafanye 1) kwa nia njema (kufanya kile ambacho ni cha uaminifu, haki, na kisheria), 2) kwa uangalifu ambao mtu mwenye busara katika nafasi kama hiyo angechukua chini ya hali kama hiyo, na 3) kwa njia ambayo mkurugenzi au afisa anaamini kuwa ni kwa manufaa ya shirika lisilo la faida. | 24.03A.495(1)<br>24.03A.590(1) |
| ● Wakurugenzi wa bodi na maofisa wote, katika kuchukua hatua za bodi, wanaweza kutegemea ushauri au taarifa zinazotolewa na wataalamu kama vile CPA, wakili, wafanyakazi wenye sifa, au wataalamu wengine. | 24.03A.495(3)<br>24.03A.590(3) |
| ● Maafisa wa bodi pia wana wajibu wa kuwaambia wakuu wao au bodi kwa ujumla taarifa zinazojulikana kuwa nyenzo (muhimu), na taarifa kuhusu ukiukaji wa sheria au uvunjaji (ukiukaji) wa wajibu. | 24.03A.590(2) |

Imesasishwa Julai 7, 2022

Nonprofit Association of Washington

Learn. Advocate. Collaborate.